Ishara ya kukabiliana na ukoloni

Taarifa

Utekelezaji wa muona wa ishara yetu ya kumbukumbu ya kukabiliana na ukoloni katika eneo la wazi, mbele ya jengo la Berlin Global Village katika madhihirisho ya kuweka wazi matukio ya kikoloni kwa njia ya sanaa ili kuifikia jamii husika kimataifa. Uratibu wa kugombea nafasi ya msanii atakayeunda ishara lengwa.

Wahamasishaji na Wafadhili wa mradi

Berlin Global Village gGmbH (BGV)
wakishirikiana na ofisi ya sanaa katika anga za umma ya Kulturwerk GmbH ya shirika la bbk berlin

Washiriki

Jumuiya ya vyama vya kiraia ambavyo vinashughulikia masuala ya ukoloni:

- AfricAvenir e.V.
- Afrika-Rat Berlin-Brandenburg e.V.
- AFROTAK TV cyberNomads
- Berlin Postkolonial e.V.
- DaMigra e.V.
- Decolonize Berlin e.V.
- Initiative Schwarze Menschen in Deutschland ISD-Bund e.V.
- moveGLOBAL e.V.

Washiriki wengine:

- Wilaya ya Neukölln, Sekta ya utamaduni
- KINDL - Zentrum für zeitgenössische Kunst
- Black Berlin Biennale (Kipupwe 2024)

Wafadhili wa mradi

Beauftragte der Bundesregierung für Kultur und Medien (BKM)
Senatsverwaltung für Kultur und Europa

Uratibu wa mchakato na uchunguzi wa awali

Oscar Ardila, Stefan Krüskemper
Wafanya kazi wenza: Salwa Aleryani, Géraldine Makazamba Ngolo, Katinka Theis

Usajili wa wasanii wa kugombea nafasi ya kuunda ishara husika

Nafasi ya kiti cha kugombea kwa kumtafuta msanii bobezi itatangazwa kimataifa na mchakato huo utafanyika kwa awamu mbili. Mashindano ya wagombezi wasanii hufanyika kwa mujibu wa waandaaji wa mwongozo unaotumika katika mashindano (RPW 2013). Lugha zitakazotumika katika shindano ni Kijerumani na Kiingereza. Hati za mashindano zipo katika lugha ya Kijerumani na Kiingereza. Maombi yote ya wasanii watakaotaka kushiriki, ni lazima pia yaandikwe na kuwasilishwa katika lugha ya Kijerumani au Kiingereza.

Wasanii wote watakaotaka kushiriki wanaweza kushiriki. Ni lazima washiriki wote watakaogombea wawe wasanii bobezi wenye taaluma ya sanaa.
Kwa ajili ya uthibitisho zinahitajika nakala za A4 zisizozidi kurasa mbili bila picha. Ikiwa msanii hana mafunzo kutoka katika chuo cha sanaa au katika taasisi inayolingana, basi inambidi awe na uthibisho wa mazoezi na uzoefu endelevu wa kitaalam alioufanya katika miradi kadhaa. Zaidi ya hayo, uanachama katika kikundi cha sanaa uwe kama ushahidi wa kuthibitisha utaalam. Ustahiki wa kushiriki utathibitiwa na usajili.

Washiriki wote watachukuliwa kwa usawa katika ufikiaji wa shindano na mchakato mzima. Masharti kwa washindani na tarehe ya mwisho ya kutuma maombi itakuwa ni sawa kwa washindani wote, na taarifa itakayotolewa kwao wote itakuwa sawa katika wakati sawa. Kwa taratibu zinazojulikana, majina halisi ya washiriki hayatatajwa mpaka mwishoni mwa shindano, ambapo majina halisi yatatangazwa baada ya uamuzi wa mwisho wa waamuzi.

Tukio na malengo

Ni kwa muda mrefu sasa ukoloni wa Wajerumani na madhara yake vimekuwa vikifumbiwa macho na kupuuzwa nchini Ujerumani.

Hata hivyo, mashirika kadhaa yamekuwa yakiingilia kati suala hili, hasa kukabiliana ipasavyo na maangamizi ya jamii nchini Namibia na uthibitisho usiowekwa wazi kwa masalia ya binadamu katika kumbukumbu za vitengo vya madawa na katika nyanja za elimu pamoja na maelfu na maelfu ya mali kale za kitamaduni katika majumba ya makumbusho ya ethnologia. Mashirika hayo yameanzisha mchakato ambao sasa pia umefika bungeni. Ili kushughulikia uhusiano kati ya ukoloni na ushirikiano wa maendeleo, Berlin Global Village gGmbH, kama mmiliki wa eneo la kumbukumbu lililoko jijini Berlin ambapo sera ya maendeleo hujadiliwa na mashirika ya diaspora hukutana. Berlin Global Village gGmbH imeandaa shindano la kimataifa la sanaa lenye awamu mbili kwa ajili ya kumpata msanii atakayeunda ishara ya kumbukumbu ya ukoloni.

Lengo la shindano ni utambuzi wa ishara ya ukumbusho wa ukoloni ambayo itatengenezwa bila muingiliano kutoka nje.
Pamoja na ukumbusho huo, Berlin Global Village itaweka ishara hiyo kama mahali pa kutafakaria masuala ya ukoloni kwa wana Berlin na waigizaji wa kimataifa. Pia eneo la zamani la kutengenezea bia ya Kindl-Areal, litatumika kama mahali ambapo mipango mbalimbali ya mashirika ya kijamii wilayani Neukölln bila kusahau watu wanaotoka nje ya wilaya hiyo ambao wana fursa ya kulitumia ili kufanya kazi za ushirikiano wa maendeleo yenye tija, kwa hivyo mahali hapo pataandaliwa kama sehemu inayolenga makumbusho ya ukoloni.

Shindano hilo la sanaa, litakaloambatanishwa na programu za elimu zinazofadhiliwa na serikali ya Ujerumani kupitia Kamishna kwa wa sekta ya utamaaduni na vyombo vya habari. Utekelezaji wa kumbukumbu hiyo unafadhiliwa na Jimbo la Berlin kupitia Idara ya Seneta wa masuala ya Utamaduni na Ulaya mkoani Berlin.

Kituo na sehemu ya kutanyia kazi

Katika eneo la zamani la kiwanda cha kutengeneza bia ya Kindl wilayani Neukölln, mnamo Machi 2021 shirika lisilo la serikali la Berlin Global Village gGmbH (BGV) lilifungua katika eneo hilo sehemu ya pamoja ya kukutania, kufanyia mijadala ya masuala ya haki na maendeleo ulimwenguni: "Berlin Global Village".

Anwani:
Berlin Global Village gGmbH
Am Sudhaus 2
D-12053 Berlin

Berlin Global Village inatoa nafasi za ofisi takriban vyumba 50 ambamo vyama vya siasa za maendeleo, vyama vya diaspora, wanaharakati kutoka vyama vidogo vidogo huru hadi mashirika makubwa yasiyo ya kiserikali (NGOs) namashirika shirikisho ya serikali hata ya mikoani. Pamoja na vyumba vya matukio na semina, maktaba ya vifaa vya kuchezea, masuala ya digitali, maktaba ya media, nyumba ya sanaa na mkahawa wa kubadirishana mawazo, kuna matoleo mengi kwa sera ya maendeleo na mashirika ya kiraia ya wahamiaji wanaoishi nje ya nchi. Kituo kinatoa huduma mbali mbali za maendeleo na masuala ya wahamiaji.

Preview architecture office Anne Lampen

Kwa madhumuni haya, Berlin Global Village ilipata haki za urithi wa ujenzi wa majengo mawili yaliyokuwa yanamilikiwa na kiwanda cha bia cha Kindl. Majengo mawili yaliyokuwa yamechakaa yalibomolewa na badala yake kujenga majengo mawili mapya mnamo mwezi wa Machi mwaka 2021. Ofisi ya msanifu jenzi Anne Lampen walibuni muundo mpya na ukarabati wa jengo zee. Katika majengo yote mawili, jengo jipya na jengo la zamani la matofali ya kuchoma ghorofa ya chini inatumika kama sehemu ya kufanyia matukio ambayo pia inaweza kukodishwa na watu kutoka nje. Pia ofisi zilizopo ghorofa ya juu zinaweza kukodishwa na mashirika binafsi (NGOs) kwa muda mrefu.

Diagram with approximate dimensions Preview architecture office Anne Lampen

Katikati au mbele ya majengo haya mawili ya BGV patasimamishwa ishara ya kumbukumbu ya ukoloni kama kitovu cha kimsingi kuhusu uhusiano wa Nord-Süd (Kaskazini-Kusini) kisanii pakiwepo pia kutokomeza ukoloni/ukoloni mambo leo. Eneo lililoandaliwa la kufanyia kazi ambapo ndipo itakaposimamishwa ishara ya kumbukumbu za ukoloni. Eneo Hilo litakuwa wazi siku nzima na wageni wanakaribishwa, pia litaonekana vizuri kutoka eneo jirani wazi la jiji.

Eneo la mbele ya Berlin Global Village linaweza kutumiwa kwa kazi za sanaa. Sehemu wazi mbele na katikati ya jengo jipya na jengo la zamani ni muhumu, inavutia na inapendeza, na paa tambarare linaunganisha jengo, ndipo penye lango kuu la kuingilia. Sehemu ya kuingia kuunganisha nje na ndani ya majengo. Miundo mbinu iliyoundwa kipekee kwa matumizi ya ndani haihitajiki.

Aina zote za sanaa za kisasa zinaweza kutengenezwa. Mpango wa kufanya kazi kwa kutumia maji haujahusishwa. Ishara ya kudumu ya ukumbusho wa ukoloni inatarajiwa kuwepo kwenye eneo hilo.

Lengo la mashindano hayo ni kupata mawazo mazuri ya sanaa (hatua ya kwanza) na miundo (hatua ya pili) kwa ajili ya eneo la kazi ambalo lina vigezo vya eneo na mpangilio wake. Aina zote za sanaa zinakaribishwa. Mamlaka ya tuzo za BGV inalenga kuendelea na shindano hilo kulingana na mapendekezo ya waamuzi wa shindano.

Usajili na watakaochaguliwa

Mwisho wa kujisajili/kutuma maombi ni siku ya Jumapili tarehe 07.05.2023 saa 23:59 muda wa Ulaya ya kati. Maombi yatumwe katika nakala za PDF zisizozidi kurasa tatu kupitia kiunganisho cha tovuti/link ifuatayo: https://hidrive.ionos.com/upl/2dHIvi08

Maombi ya kushiriki yanapaswa kuwa na nakala za PDF zenye ukubwa wa A4 na zisizidi MB5 kama ifuatavyo:

- Fomu ijazwe na majina kamili (wasanii, vikundi vya wasanii), anwani halali ya posta, anwani ya barua pepe na namba ya simu (fomu ya maombi imeambatinishwa)

- CV yenye uthibitisho wa utaalamu wa msanii (zisizidi kurasa mbili za A4 katika nakala ya PDF, bila picha)

Utambulisho wa faili la PDF: jina la ukoo.pdf/sirname.pdf (mfano: schumacher.pdf)

Vigezo vya kushiriki vitakaguliwa wakati wa usajili. Vigezo muhimu ni stashahada kutoka chuo kikuu cha sanaa au kazi inayolingana, bila kusahau CV kama uthibitisho wa kazi ya utaalamu wa sanaa na orodha ya maonyesho au uanachama katika kikundi cha sanaa. Wanachama wote wa kikundi cha wasanii lazima wawe wasanii waliobobea na wenye taaluma ya sanaa. CV yenye orodha ya maonyesho na miradi isiyozidi kurasa 2 za A4 bila picha, itafaa kuwa uthibitisho wa utaalamu na ubobezi. Ikiwa mwombaji hana mafunzo kutoka chuo kikuu cha sanaa au kutoka katika taasisi inayolingana, maonyesho au mradi lazima athibitishe kazi endelevu za kisanii ambazo zinakidhi viwango vya kitaaluma na ubobezi. Zaidi ya hayo, uanachama katika kikundi cha wasanii utazingatiwa kama uthibitisho wa utaalumu wa msanii.

Waombaji watakaokidhi vigezo watapewa taarifa ya kushiriki katika shindano kwa njia ya kidigitali mnamo tarehe 15 Mei 2023. Makampuni hayaruhusiwi kutuma maombi. Masharti hayo hayo yatazingatiwa kwa vikundi vya wasanii vitakavyojisajili zaidi ya mara moja.

Uwezo unaotakiwa

Katika awamu ya kwanza ya shindano, washiriki wanaombwa kuwasilisha wazo la sanaa katika mchoro ukiwa umeambatanishwa na kuzingatia ishara lengwa. Hakuna maelezo ya muundo au maelezo ya kiufundi yanayotarajiwa.

Jopo la waamuzi litachagua washiriki 20 watakaoingia awamu ya 2, ambapo ufafanuzi wa kina wa muundo kwa ajili ya utekelezaji unatarajiwa zaidi na utatiliwa maanani.

Wasanii ambao watashiriki kama kikundi watawasilisha muundo wa sanaa ambao umeundwa mahususi kwa ajili ya shindano hilo.

Fedha ya gharama za awali

Washiriki katika awamu ya kwanza ya shindano hawatalipwa fedha yoyote kwa ajili ya gharama za awali. Katika awamu ya 2 ya shindano, washiriki watapata fedha ya kiasi cha jumla ya €4,000.00 ikijumuisha gharama zote za ziada, ikiwa kazi itakayowasilishwa itakidhi masharti ya shindano. Hakuna pesa zitakazotolewa kama tuzo.

Jumla ya gharama

Kiasi cha fedha zilizotengwa kwa kazi hii jumla ni 750.000,00 € itakayojumuisha gharama zote za ziada zitakazojitokeza katika ujenzi wa sanaa lengwa (yakiwemo malipo ya msanii, vifaa na gharama za ufundi).

Waamuzi wa shindano

Waamuzi wenye taaluma ya sanaa:

- Kristina Leko (Chuo kikuu cha sanaa cha Berlin, taaluma ya sanaa)
- Prof. Dr. Chika Okeke-Agulo (Chuo kikuu cha Princeton, taaluma ya sanaa)
- María Linares (taaluma ya sanaa)
- t.b.a.

Waamuzi wataalamu:

- Michael Küppers-Adebisi (Berlin Global Village gGmbH, muwakilishi wa mfadhili)
- Prof. Dr. Walter Mignolo (Chuo kikuu cha Duke)
- t.b.a.

Wawakilishi wa kudumu:

- t.b.a.

Deadlines and dates

07.05.23	Mwisho wa kutuma maombi
15.05.23	Utoaji wa nyaraka za zabuni
14.06.23	Tarehe ya mwisho ya maswali yaliyoandikwa awamu ya kwanza
23.06.23	Kujibu maswali ya awamu ya kwanza
13.08.23	Uwasilishaji wa rasimu za awamu ya kwanza kidigitali
16./17.09.23	Kikao cha waamuzi awamu ya kwanza
18.09.23	Taarifa kwa washiriki walioteuliwa kuingia awamu ya pili
30.10.23	Ushauri wa awamu ya pili
31.10.23	Kongamano
12.11.23	Tarehe ya mwisho ya maswali yaliyoandikwa kwa awamu ya pili
24.11.23	Kujibu maswali ya awamu ya pili
07.01.24	Tarehe ya mwisho ya uwasilishaji wa rasimu za awamu ya pili
27.01.24	Kikao cha waamuzi awamu ya pili
28.02.24	Kuonyesha miundo itayowasilishwa kutoka awamu ya pili

Mawasiliano

artcontest@berlin-global-village.de

More information

Website: https://www.berlin-global-village.de
Podcast: https://youtu.be/x8jJCVP6xus
Facebook: www.facebook.com/BerlinGlobalVillage
Instagram: @berlinglobalvillage

Awarding authority

berlin global village

Cooperation partners

AFRICAVENIR

Afrika-Rat
Dachverband afrikanischer Vereine und Initiativen Berlin-Brandenburg

AFROTAK TV
cyberNomads

BERLIN POSTKOLONIAL

DaMigra
Dachverband der Migrantinnenorganisationen

DECOLONIZE BERLIN

isd

move GLOBAL

Project sponsors

Die Beauftragte der Bundesregierung für Kultur und Medien

Senatsverwaltung für Kultur und Europa
BERLIN

Tafadhali jaza fomu hii:

Usajili wa shindano la sanaa ya ishara ya ukumbusho wa ukoloni

Msanii au Kikundi cha wasanii
Jina
Anwani (mtaa, mji/kitongoji, nchi)
Anwani ya barua pepe
Namba ya simu

Ijazwe na vikundi vya wafanya kazi tu
Washiriki wengine
Washiriki wengine
Washiriki wengine
Washiriki wengine

Tafadhali ambatanisha CV ya usanii na uthibitisho wa ubobezi na taaluma ya washiriki wote (zisizidi kurasa mbili za A4, bila picha, muundo wa nakala uwe PDF)

Mwisho wa kutuma usajili ni Jumapili, tarehe 07. Mei 2023, saa 23:59 **muda wa Ulaya ya kati.**
Tuma kupitia **:** https://hidrive.ionos.com/upl/2dHIvi08